Bomas of Kenya

Bomas of Kenya ni makumbusho ya utamaduni wa makabila ya Kenya yanayoonyesha nyumba na vijiji vya kimila kutoka pande nyingi za nchi.

Kijiji cha Waluo kwenye Bomas of Kenya.

Kuna makumi ya nyumba zilizopangwa pamoja kufuatana na maeneo asilia; kwa mfano Waembu, Wakalenjin, Wakamba, Wakikuyu, Wakisii, Wakuria, Waluhya, Waluo, Wamaasai, Wamijikenda au Wataita.

Getini kuna ukumbi mkubwa wenye nafasi 3,500 uliojengwa kwa namna ya kufanana na nyumba za kimila na katika ukumbi huo kuna maonyesho ya ngoma za makabila ya Kenya. Maonyesho hayo hutembelewa na wananchi na pia watalii.

Ukumbi mkubwa ulikuwa pia mahali pa mikutano ya pekee. Mkutano wa kutunga katiba mpya ulifanyika hapo baada ya uchaguzi wa rais Mwai Kibaki lakini katiba hii haikukubaliwa baadaye na serikali.

Tazama pia

- Gedi
- Jumba la Mtwana
- Makumbusho ya Garissa
- Makumbusho ya Kabarnet
- Makumbusho ya Kapenguria
- Makumbusho ya Kitale
- Makumbusho ya Narok
- Makumbusho ya reli Nairobi

Makala hii kuhusu maeneo ya Kenya bado ni **mbegu**.
Je unajua kitu kuhusu **Bomas of Kenya** kama historia yake, biashara, taasisi zilizopo, watu au utamaduni?
Labda unaona habari katika wikipedia ya Kiingereza au lugha nyingine zinazofaa kutafsiriwa?
Basi unaweza kuisaidia Wikipedia kwa kuihariri na kuongeza habari (https://sw.wikipedia.org/w/index.php?stub&title=Bomas_of_Kenya&action=edit).

Rudishwa kutoka "https://sw.wikipedia.org/w/index.php?title=Bomas_of_Kenya&oldid=1112046"

Ukurasa huu umebadilishwa kwa mara ya mwisho tarehe 3 Mei 2020, saa 07:57.

Maandishi yanapatikana chini ya leseni ya Creative Commons Attribution-ShareAlike License; matakwa mengine yanaweza kutakiwa. Tazama maelezo zaidi ya Matakwa ya Utumiaji.